# SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR
# WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

## MUHUTASARI WA ELIMU YA MSINGI

DARASA LA I – III

# SOMO LA KISWAHILI

2022

© TEZ, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, 2022

Toleo la Kwanza 2022

Imesanifiwa na kuandaliwa na:

Taasisi ya Elimu ya Zanzibar (TEZ)

S.L.P 840,

Mazizini, Zanzibar

Barua Pepe: info@zie.go.tz
Tovuti: www.zie.go.tz
Simu: +255-24-2230193

ISBN:**978-9912-754-58-4**

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupiga chapa au kutoa kopi nyaraka hii kwa namna yoyote ile bila ya idhini ya Taasisi ya Elimu ya Zanzibar.

# YALIYOMO


**DIBAJI**........v

**SHUKURANI**........v

**1.0 UTANGULIZI**........vi

1.1 Falsafa ya Elimu ya Zanzibar........vi

1.2 Madhumuni ya Elimu Zanzibar........vi

1.3 Malengo ya Elimu ya Msingi........vii

1.4 Sababu za Kupitia Mtaala wa Msingi........viii

1.5 Umuhimu wa Kujifunza Somo la Kiswahili........viii

1.6 Matokeo ya Jumla katika Somo la Kiswahili Darasa la I-III........viii

**2.0 MUUNDO WA MUHUTASARI**........viii

2.1 Kurasa za Awali........viii

2.2 Jaduweli la Muhutasari........ix

2.2.1 Mada........ix

2.2.2 Matokeo Mahususi ya Kujifunza........ix

2.2.3 Mbinu za Kujifunzia........ix

2.2.4 Nyenzo za Kujifunzia........ix

2.2.5 Upimaji........ix

2.2.6 Vipindi........x

2.3 Mawanda na Mtiririko........x

**DARASA LA I**........1

Matokeo ya Jumla ya Kujifunza kwa Darasa la I........2

**DARASA LA II**........19

Matokeo ya Jumla ya Kujifunza kwa Darasa la II........20

**DARASA LA III**........36

Matokeo ya Jumla ya Kujifunza kwa Darasa la III........37

# DIBAJI

Muhutasari wa somo la Kiswahili wa darasa la I-III wa mwaka 2022, unatokana na mabadiliko makubwa ya kielimu yaliyofanywa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (WEMA) ambayo yamehusisha kazi ya upitiaji wa Mtaala wa Elimu ya Maandalizi na Msingi ulioandikwa mwaka 2019. Madhumuni ya kupitia mtaala huo ni kuufanya uendane na maendeleo ya sayansi na teknolojia, ushindani wa soko la ajira pamoja na mabadiliko ya kiuchumi ulimwenguni kama inavyoelezwa katika nyaraka mbalimbali za Serikali ikiwemo Sera ya Elimu ya Zanzibar.

Kutokana na mabadiliko ya mfumo wa elimu Zanzibar, yaliyopelekea kurejeshwa kwa darasa la saba ikiwa ni miongoni mwa uimarishaji wa elimu ya msingi, kwa sasa elimu ya msingi itakuwa ni miaka 7 badala ya miaka 6 ya awali. Kwa kuzingatia mabadiliko hayo, WEMA kupitia Taasisi ya Elimu ya Zanzibar (TEZ) imeandika muhutasari wa somo la Kiswahili ili kukidhi mahitaji ya taaluma hiyo. Kwa hivyo, muhutasari huu umekusanya mada za somo la Kiswahili ambazo zinaendana na maudhui na muktadha wa somo hili. Kazi ya uandishi wa muhutasari huu imejumuisha wadau mbalimbali wa elimu katika ngazi tafauti hususan elimu ya msingi. WEMA kupitia TEZ imehakikisha kuwa muhutasari umezingatia vyema maoni ya wadau hao, pamoja na mapitio ya machapisho mbalimbali kutoka nchi nyengine zinazofanana kijiografia, idadi ya wakaazi na mifumo ya elimu.

WEMA inatoa shukurani za dhati kwa wadau wote waliochangia katika kuandaa muhutasari huu wa somo la Kiswahili wa darasa la I-III wakiwemo; Wajumbe wa Bodi ya Ushauri ya Taasisi, Uongozi na Watendaji wote wa TEZ, Jopo la Wataalamu, Wakuza Mitaala, Walimu na Wastaafu mbalimbali wa WEMA walioshiriki katika matayarisho ya muhutasari huu hadi kukamilika kwake.

Ni matumaini ya WEMA kuwa, muhutasari huu utatumika kwa skuli zote za Zanzibar za serikali na binafsi pamoja na watekelezaji wengine katika ngazi ya elimu ya msingi.

Khamis A. Said.
Katibu Mkuu,
Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali,
Zanzibar.

# SHUKURANI

Taasisi ya Elimu ya Zanzibar inatoa shukurani za dhati kwa Mh. Leila Muhamed Mussa; Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Mh. Ali Abdulghulam Hussein; Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Nd. Khamis Abdulla Said; Katibu Mkuu WEMA, Dkt. Mwanakhamis Adam Ameir; Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar na Dkt. Abdullah Ismail Kanduru; Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya TEZ.

Shukurani za pekee ziwaendee wakuu wa divisheni za TEZ, wafanyakazi wote wa TEZ na Wajumbe wa Bodi ambao walikuwa ni washiriki wa kazi hii ya utayarishaji wa Muhutasari. Pia, shukurani ziwaendee maafisa wa ngazi tafauti katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kutumia muda wao na kutoa maoni kuhusu mambo yanayopaswa kuzingatiwa katika uandaaji wa muhutasari huu. Kwa kuongezea, TEZ inawashukuru walimu wote, wazazi na wanafunzi kwa kushiriki katika kazi hii.

Aidha, TEZ inazishukuru taasisi mbalimbali kwa kuwaruhusu watendaji wao kufanya kazi kwa pamoja. Taasisi zenyewe ni Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Chuo cha Kikuu cha Abdulrahman Al-Sumait, Idara ya Mafunzo ya Ualimu, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu, Baraza la Mitihani la Zanzibar, Chuo cha Kiislamu, Idara ya Elimu ya Maandalizi na Msingi, Idara ya Elimu ya Sekondari, Jumuiya ya Skuli Binafsi. Taasisi nyengine ni Madrasa Early Childhood Programme Zanzibar, Mamlaka ya Mji Mkongwe, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar, Mamlaka ya Udhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar, Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha, Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja na Ofisi ya Mufti Mkuu na Taasisi nyengine zilizoshiriki katika kufanikisha upatikanaji wa Mihutasari ya Elimu ya Msingi.

Mwisho, TEZ inatoa shukurani za dhati kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na washirika wa maendeleo hususan Global Partnership for Education (GPE) kwa kutoa mchango wao wa hali na mali katika kukamilisha kazi hii.

Abdalla M. Mussa.
Mkurugenzi Mtendaji,
Taasisi ya Elimu ya Zanzibar,

Zanzibar.

# UTANGULIZI

Muhutasari wa somo la Kiswahili umeandaliwa kwa wanafunzi wa darasa la I-III ambao umechukua nafasi ya muhutasari wa somo la Kiswahili kwa ngazi ya msingi darasa la I-VI wa mwaka 2009. Muhutasari huu umejumuisha sehemu ya Utangulizi, Falsafa ya Elimu ya Zanzibar, Malengo ya Elimu ya Msingi na Madhumuni ya Elimu ya Zanzibar, Sababu za kupitiwa muhutasari na umuhimu wa kujifunza somo la Kiswahili. Pia, muhutasari huu umejumuisha Matokeo ya Jumla ya Kujifunza somo la Kiswahili, Muundo wa Muhutasari, Matokeo ya Jumla ya Kujifunza kwa kila darasa pamoja na Jaduweli la Muhutasari.

## 1.1 Falsafa ya Elimu ya Zanzibar

Mfumo wa Mtaala wa Elimu ya Maandalizi na Msingi unakwenda sambamba na Falsafa ya Elimu ya Zanzibar kwa kuzingatia mila na misingi ya mfumo wa elimu hiyo.

Falsafa ya Elimu ya Zanzibar ni sawa na ile ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo imejikita zaidi na Falsafa ya Ujamaa na Kujitegemea, ambayo inamtaka kijana aweze kujitosheleza, kujiamini, kujiendeleza, kupata stadi za maisha, kuthamini usawa, kuwa mjasiriamali, kuvumbua, kudadisi, kubuni na kuweza kutathmini na kuchambua mambo.

## 1.2 Madhumuni ya Elimu Zanzibar

Yafuatayo ni madhumuni ya elimu Zanzibar:-

1. Kukuza na kudumisha tabia na desturi bora za Wazanzibari na Watanzania ili kuimarisha umoja na utambulisho wao wa kiutamaduni.

2. Kuimarisha upatikanaji na matumizi sahihi ya aina mbalimbali za maarifa, stadi na mwelekeo kwa ajili ya kuendeleza kikamilifu utu na ubora wa maisha ya jamii.

3. Kuwezesha kila mwananchi kuelewa na kuheshimu misingi ya Katiba ya Zanzibar na ya Tanzania, haki za binadamu, wajibu na majukumu ya kila raia.

4. Kuendeleza na kuhimiza matumizi bora, uangalizi na utunzaji wa mazingira.

5. Kukuza utashi na heshima ya kufanya kazi za kujiajiri na kuajiriwa inayoambatana na nidhamu kazini na utendaji kazi wenye ubora wa kiwango cha juu.

6. Kukuza na kudumisha misingi ya kuvumiliana, amani, upendo, maelewano, haki za binadamu na uhuru, umoja wa kitaifa na kimataifa kama vinavyofafanuliwa katika mikataba ya kimataifa.

### 1.3 Malengo ya Elimu ya Msingi

Yafuatayo ni malengo ya elimu ya msingi ya Zanzibar:

1. Kuwawezesha watoto wote wenye umri wa kwenda skuli kujenga na kudumisha misingi imara ya stadi za kusoma, kuandika, kuhesabu, kubuni na kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili, Kiingereza na lugha nyengine za kigeni.

2. Kuwawezesha wanafunzi kuelewa matumizi ya Sayansi na Teknolojia ili kutambua mchango wake katika maendeleo ya taifa lao na ulimwengu.

3. Kuweka, kuendeleza na kudumisha wanafunzi misingi imara ya stadi za kufikiri na udadisi ili kuelewa mazingira yao na mahusiano ya kijamii.

4. Kuwawezesha wanafunzi kuelewa jinsi matukio yaliyopita yanavyoathiri matukio ya wakati uliyopo na ya wakati ujao.

5. Kugundua vipaji vya kila mwanafunzi wakiwa na umri mdogo ili kuvidumisha na kuviendeleza.

6. Kuweka misingi imara ya stadi za kuchunguza, kutafakari, na kushirikiana katika kutatua matatizo yanayodumaza maendeleo binafsi ya wanafunzi katika jamii yao.

7. Kuwaandaa wanafunzi kujiunga na elimu ya sekondari.

8. Kuwawezesha wanafunzi kukuza uwezo wao kiakili na utashi wa kujitafutia maarifa.

9. Kuwazoesha wanafunzi kufanya shughuli za uzalishaji mali kukuza ari yao katika kutekeleza majukumu ya kijamii.

10. Kuwawezesha wanafunzi kutambua na kuenzi umoja wa taifa lao na kuendeleza mashirikiano baina ya Taifa lao na Mataifa mengine.

11. Kuwawezesha wanafunzi kujenga maadili mema kiroho, kiutamaduni na kiitikadi ili kukuza uzalendo na kufahamu hali ya nchi yao kihistoria, kisiasa na kijamii.

12. Kukuza na kudumisha nidhamu binafsi ya mwanafunzi, kuheshimu usawa wa kijinsia na kulinda afya zao na za watu wengine.

13. Kuwawezesha wanafunzi kujenga tabia za umaridadi na unadhifu pamoja na matumizi bora ya muda wao wa mapumziko.

14. Kukuza upendo baina ya wanafunzi, kutunza mazingira wanayoishi kulingana pamoja na utashi wao.

## 1.4 Sababu za Kupitiwa Mtaala wa Msingi

Mnamo mwaka 2019, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilifanya mapitio ya Mtaala wa Elimu ya Maandalizi na Msingi. Madhumuni yalikuwa ni kuufanya mtaala uendane na maendeleo ya sayansi na teknolojia, ushindani wa soko la ajira pamoja na mabadiliko ya kiuchumi ulimwenguni, kama inavyoelezwa katika nyaraka mbalimbali za Serikali ikiwemo Sera ya Elimu ya Zanzibar. Sera hiyo inalenga kuimarisha ubora na muundo wa elimu ili kuwa na muunganiko mzuri unaoanzia Elimu ya Maandalizi, Msingi na Sekondari kwa kukidhi matarajio ya walengwa na jamii yao. Miongoni mwa mabadiliko yaliyopendekezwa ni kuwa na miaka saba (7) ya elimu ya msingi badala ya miaka sita (6) ya awali.

## 1.5 Umuhimu wa Kujifunza Somo la Kiswahili

Kiswahili kama lugha nyengine ni njia muhimu katika mawasiliano nchini Zanzibar, Kiswahili ni lugha ya Taifa na huzungumzwa na Wazanzibari wote. Vilevile, Kiswahili ndiyo lugha kuu ya kuendeshea shughuli za Serikali ikifuatiwa na Kiingereza.

Katika elimu, Kiswahili ni lugha ya kufundishia katika ngazi za Elimu ya Maandalizi na Msingi. Kadhalika, Kiswahili ni lugha ya kuendeshea biashara na kukuza uchumi wa mtu binafsi na Serikali kwa ujumla. Zaidi ya hayo, lugha hii ni kioo cha utamaduni wa Zanzibar na kichocheo cha uzalendo na umoja wa nchi. Aidha, Kiswahili huwaunganisha Wazanzibar na jamii jirani na hivyo kustawisha uhusiano mwema wa Tanzania, Afrika Mashariki na mataifa mengine ulimwenguni.

Muhutasari huu utatumiwa na walimu na wanafunzi katika skuli za msingi. Unachukua nafasi ya Muhutasari wa Kiswahili uliotolewa na Serikali mwaka 2009. Muhutasari huu unazingatia stadi zote nne za lugha. Stadi hizo ni kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika. Stadi hizi ni muhimu katika kumjenga na kumuimarisha mwanafunzi katika kukabiliana na ulimwengu wa kidijitali katika ngazi mbalimbali za kielemu na harakati za kimaisha.

## 1.6 Matokeo ya Jumla ya Kujifunza Somo la Kiswahili Darasa la I-III

Baada ya kusoma somo la Kiswahili kwa ngazi ya msingi chini, mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-

1. Kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili kwa njia ya mazungumzo na maandishi.
2. Kusikiliza, kusoma na kufahamu habari mbalimbali.
3. Kuandika matini ndogondogo kwa kutumia lugha ya Kiswahili.

## 2.0 MUUNDO WA MUHUTASARI

Muhutasari huu una sehemu kuu mbili: Kurasa za awali na Jaduweli la muhutasari.

## 2.1 Kurasa za Awali

Sehemu hii inajumuisha Utangulizi wa Muhutasari, Falsafa ya Elimu ya Zanzibar, Malengo ya Elimu ya Msingi na Madhumuni ya Elimu Zanzibar, pamoja na umuhimu wa kujifunza somo la Kiswahili. Pia, kuna matokeo ya jumla ya kujifunza somo hili.

Vipengele vyengine ni maelezo kuhusu mawanda na mtiririko wa mada zilizomo, matokeo ya jumla ya darasa husika na ufafanuzi wa vipengele vya jaduweli la ujifunzaji.

### 2.2 Jaduweli la Muhutasari

Sehemu hii inaonesha utaratibu wa ujifunzaji uliobainishwa katika majadweli matatu yaliyobeba maudhui ya darasa la I hadi la III. Kila jaduweli limeanza na orodha ya matokeo ya jumla ya kujifunza kwa darasa linalohusika. Baada ya matokeo ya jumla linafuata jaduweli la ujifunzaji lenye safuwima saba zenye stadi, mada, Matokeo Mahususi ya Kujifunza, Mbinu za Kujifunzia, Nyenzo za Kujifunzia, Upimaji na Vipindi kwa kila mada ndogo. Yafuatayo ni maelezo ya kila kipengele.

#### 2.2.1 Mada

Mada zimejikita katika mawanda ya ufundishaji na ujifunzaji wa mada husika.

#### 2.2.2 Matokeo Mahususi ya Kujifunza

Kila mada ndogo huonesha matokeo mahususi ya kujifunza. Matokeo hayo yanaelezea maarifa, ujuzi na mwelekeo ambao kila mwanafunzi anapaswa kujifunza katika mada ndogo inayohusika. Matokeo mahususi ndiyo yanayotumiwa kufanyia upimaji, ambayo hudokeza viashiria vinavyojenga umahiri. Kwa kawaida, wakati wa kujifunza mwanafunzi huanza kuonesha viashiria hivyo akiwa darasani. Hivyo, kila mwanafunzi anatakiwa kuyafikia matokeo mahususi yaliyotajwa.

#### 2.2.3 Mbinu za Kujifunzia

Safuwima hii imejumuisha mbinu shirikishi za kutumia katika kujifunzia mada za somo hili. Mbinu hizo ni kama; maswali na majibu, bungua bongo, onesho mbinu, igizo dhima na mazoezi ya vitendo. Haya ni mapendekezo ya mbinu ambazo zimethibitika kuongeza ushiriki wa wanafunzi katika vitendo vya kujifunza. Mwalimu anashauriwa kutumia mbinu nyengine shirikishi atakazoona zinafaa kufundishia kulingana na mazingira yake.

#### 2.2.4 Nyenzo za Kujifunzia

Nyenzo za kujifunzia huendana na mbinu za kujifunzia, matokeo mahususi ya kujifunza, mada ndogo na mahitaji ya kila mada ndogo. Hata hivyo, nyenzo zilizoorodheshwa ni mapendekezo tu, mwalimu anashauriwa kuwa mbunifu katika kutengeneza nyenzo zinazotokana na mazingira halisi au malighafi za bei nafuu. Aidha, mwalimu ashirikiane na wanafunzi kubuni na kutengeneza zana za kujifunzia kwa kutumia malighafi zilizomo katika mazingira yao.

#### 2.2.5 Upimaji

Katika safuwima hii, zimependekezwa njia za kupima iwapo mwanafunzi amefikia matokeo mahususi ya kujifunza kwa mada husika. Kila siku, wiki, mwezi, muhula na mwisho wa mwaka wa masomo mwalimu anahimizwa kupima maendeleo ya kila mwanafunzi kwa kutumia njia mbalimbali. Njia hizo za upimaji ni kama vile upimaji

binafsi, uchunguzi, mkoba wa kazi, orodha hakiki, maswali na majibu na mazoezi. Wakati wa kuzitumia njia hizo, ni vyema mwalimu akazingatia mapendekezo ya upimaji yaliyomo katika muhutasari pamoja na kuzingatia mahitaji ya kila mwanafunzi.

### 2.2.6 Vipindi

Hii ni safuwima inayoonesha idadi ya vipindi kwa kila mada inayofundishwa. Idadi hiyo imefikiwa baada ya kujumlisha vipindi vya somo kwa mwaka wa masomo (siku 210) kwa kila darasa. Jumla hiyo imegawika kwa idadi ya mada ndogo zilizomo katika muhutasari ili kupata wastani wa vipindi kwa kila mada ndogo. Makadirio haya yanaweza kubadilishwa na mwalimu kulingana na mazingira ya ujifunzaji wa mada inayohusika. Mabadiliko hayo yasizidi idadi ya vipindi anavyotakiwa mwanafunzi kufundishwa kwa mwaka. Somo la Kiswahili lina vipindi sita (6) kwa wiki kwa darasa la I na la II, darasa la III lina vipindi vitano (5) kwa wiki. Kuanzia Jumatatu hadi Alhamisi, muda wa kipindi kimoja ni dakika arobaini (40) kwa mkondo wa asubuhi na dakika thelathini na tano (35) kwa mkondo wa mchana. Siku ya Ijumaa kila kipindi kitachukua dakika thelathini (30) tu. Utawala wa skuli unatakiwa kufidia muda wa masomo utakaopotea kutokana na dharura zitakazojitokeza.

### 2.3 Mawanda na Mtiririko

Mada zimepangwa kulingana na makuzi ya wanafunzi ya kiakili, kiroho, kimwili na kihisia. Pia uwezo wao wa kujifunza, umuhimu wa somo katika shughuli za kiuchumi katika jamii yao na kutegemeana kwa mada. Aidha, mada za masuala mtambuka, hususan ujasiriamali na stadi za maisha zimezingatiwa.

Mwalimu anashauriwa kufundisha mada hizi kwa kuzingatia mazingira ya kujifunzia na muktadha utakaofaa. Jaduweli lifuatalo linaonesha mpangilio wa mada zilizopendekezwa katika Muhutasari:

| NA | MADA | MTIRIRIKO WA MADA KWA DARASA | | |
|---|---|---|---|---|
| | | DARASA LA I | DARASA LA II | DARASA LA III |
| 1. | MAWASILIANO | √ | √ | √ |
| 2. | USOMAJI | √ | √ | √ |
| 3. | MAKTABA | √ | √ | √ |
| 4. | UANDISHI | √ | √ | √ |
| 5. | SARUFI | √ | √ | √ |
| 6. | FASIHI SIMULIZI | √ | √ | √ |
| | JUMLA | 6 | 6 | 5 |

# DARASA LA I

## DARASA LA I

### Matokeo ya Jumla ya Kujifunza kwa Darasa la I

Katika kujifunza somo la Kiswahili kwa darasa la kwanza mwanafunzi aoneshe uwezo wa:

1. Kusikiliza na kufuata maelekezo kwa usahihi.
2. Kusoma na kuandika maneno na sentensi fupi kwa usahihi.
3. Kutumia maktaba kusoma vitabu na machapisho mengine.
4. Kutumia vipengele vya msingi vya sarufi ya Kiswahili katika kuzungumza na kuandika.
5. Kutumia nyimbo na vitendawili katika kujenga udadisi.

## DARASA LA KWANZA

| STADI | MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA** | **1. MAWASILIANO**<br><br>1.1 Kufuata maelekezo | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kubainisha vitendo vya maelekezo kutoka katika habari.<br>ii. Kufafanua maelekezo yanayotokana na habari aliyoisikiliza.<br>iii. Kufuata maelekezo kwa usahihi. | • Maswali na majibu<br>• Onesho mbinu<br>• Fikiri jozisha shirikisha<br>• Michezo<br>• Majadiliano<br>• Kisa mafunzo<br>• Igizo dhima | • Ubao wa sentensi<br>• Maandishi makubwa<br>• Picha za maelekezo<br>• Matini<br>• Makala<br>• Kinasa sauti | • Maswali na majibu<br>• Uchunguzi<br>• Dole gumba juu dole gumba chini<br>• Majadiliano | 12 |
| | 1.2 Kuamkia | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kuainisha | • Maswali na majibu<br>• Nyimbo<br>• Michezo | • Picha zinazoonesha vitendo vya kuamkiana | • Maswali na majibu<br>• Ugunduzi | 12 |

| STADI | MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | aina za maamkizi.<br>ii. Kubainisha maneno yanayotumika katika maamkizi.<br>iii. Kuamkia watu wa rika tafauti kulingana na muktadha. | • Fikiri jozisha shirikisha<br>• Onesho mbinu<br>• Majibizano<br>• Igizo dhima | • Kadi za maneno<br>• Modeli ya Kipaza sauti<br>• Vikaragosi | • Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano<br>• Mkoba wa kazi | |
| | 1.3 Kujitambulisha | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kutoa maelezo yake binafsi.<br>ii. Kubainisha maneno yanayotumika katika | • Onesho mbinu<br>• Majibizano<br>• Nyimbo<br>• Maswali na majibu | • Kadi za maneno<br>• Video, DVD<br>• Vikaragosi<br>• Maandishi makubwa<br>• Projekta, kompyuta | • Maswali na majibu<br>• Ugunduzi<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano | 12 |

| STADI | MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | kujieleza.<br>iii. Kujieleza. | | | | |
| | 1.4 Kuelezea hisia | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kuchunguza picha zinazoonesha hisia.<br>ii. Kuigiza hisia zinazoonesha furaha na huzuni.<br>iii. Kuhusisha hisia na matukio. | • Maswali na majibu<br>• Onesho mbinu<br>• Michezo<br>• Fikiri jozisha shirikisha<br>• Majadiliano<br>• Igizo dhima | • DVD<br>• Seti ya projekta<br>• Picha zinazoonesha hisia<br>• Karatasi za maandishi makubwa<br>• Vikaragosi<br>• Kadi za maneno | • Maswali na majibu<br>• Ugunduzi<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano | 10 |
| KUSOMA | **2. USOMAJI**<br>2.1 Kusoma kwa mazoezi | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kutamka | • Fikiri jozisha shirikisha<br>• Michezo<br>• Mazoezi | • Kapu la kadi za maneno<br>• Chati ya alama za uandishi | • Maswali na majibu<br>• Ugunduzi<br>• Uchunguzi | 16 |

| STADI | MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
| --- | --- | --- | --- | --- | --- | --- |
| | | sauti za herufi.<br>ii. Kusoma herufi, silabi na maneno.<br>iii. Kusoma sentensi fupi na ndefu kwa kuzingatia alama za uandishi. | • Nyimbo | • Kadi za alama za uandishi<br>• Ubao wa sentensi | • Majadiliano | |
| | 2.2 Kusoma kwa ufahamu | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kubainisha maneno teule.<br>ii. Kusoma habari fupi kwa | • Michezo<br>• Maswali na majibu<br>• Fikiri jozisha shirikisha<br>• Majadiliano | • Kadi za maneno<br>• Matini<br>• Makala<br>• Majarida | • Ugunduzi<br>• Maswali na majibu<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano | 16 |

| STADI | MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | ufahamu.<br>iii. Kujibu maswali kutokana na habari aliyoisoma. | | | | |
| | 2.3 Kusoma nambari 1-150 kwa maneno | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kubainisha nambari kwa maneno.<br>ii. Kulinganisha nambari na maneno ya nambari.<br>iii. Kusoma nambari kwa maneno | • Michezo<br>• Matembezi ukumbini<br>• Fikiri jozisha shirikisha<br>• Majibizano<br>• Nyimbo<br>• Mazoezi | • Kadi za maneno<br>• Kadi za maneno na nambari<br>• Kibao fumbo | • Maswali na majibu<br>• Ugunduzi<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano | 12 |
| KUSOMA | **3. MAKTABA** | **Mwanafunzi** | • Ziara ya kimasomo | • Vitabu vya | • Maswali na | 12 |

| STADI | MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 3.1 Matumizi ya maktaba | **aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kubainisha kanuni za matumizi ya maktaba.<br>ii. Kueleza umuhimu wa maktaba.<br>iii. Kutumia maktaba katika usomaji wa vitabu. | • Onesho mbinu<br>• Fikiri jozisha shirikisha<br>• Maswali na majibu<br>• Kualika mgeni | picha<br>• Karatasi za maandishi makubwa<br>• Vitabu vya maneno<br>• Vitabu vya hadithi<br>• Magazeti<br>• Makala<br>• Majarida | majibu<br>• Kadi mrejesho<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano<br>• Mkoba wa kazi | |
| | 3.2 Maktaba ya darasa | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kueleza dhana ya maktaba ya darasa. | • Onesho mbinu<br>• Fikiri jozisha shirikisha<br>• Bungua bongo<br>• Majadiliano<br>• Matembezi ukumbini | • Vitabu<br>• Vitabu vya nukta nundu<br>• Karatasi za maandishi mkubwa<br>• Vijarida<br>• Kadi za | • Maswali na majibu<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano<br>• Chemsha bongo | 12 |

| STADI | MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | ii. Kufafanua vifaa vya kusomea katika maktaba ya darasa.<br>iii. Kutumia vifaa vya kusomea katika maktaba ya darasa. | | maneno<br>• Kadi za sentensi<br>• Vipeperushi | | |
| | 3.3 Utengenezaji wa vijitabu vya kusomea watoto. | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:**<br>i. Kubainisha zana za kutengeneza vijitabu vya kusomea watoto. | • Onesho mbinu<br>• Fikiri jozisha shirikisha<br>• Maswali na majibu<br>• Nyimbo<br>• Michezo | • Manila<br>• Mikasi<br>• Kalamu<br>• Penseli<br>• Mstari<br>• Raba<br>• Pini<br>• Mashine ya pini<br>• Rangi | • Maswali na majibu<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano | 16 |

| STADI | MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | ii. Kutengeneza vijitabu vya watoto.<br>iii. Kufafanua njia za uhifadhi wa vijitabu vya watoto. | | • Gundi<br>• Misumari<br>• Karatasi<br>• Modeli ya kitabu<br>• Kamba | | |
| KUANDIKA | **4. UANDISHI**<br>4.1 Nakshi | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kuainisha nakshi nane za msingi na mabadiliko yake.<br>ii. Kubainisha herufi za nakshi nane za msingi. | • Nyimbo<br>• Michezo<br>• Fikiri jozisha shirikisha<br>• Onesho mbinu<br>• Mazoezi | • Chati ya nakshi nane za msingi<br>• Chati ya herufi kubwa na ndogo<br>• Kadi za herufi kubwa na ndogo<br>• Kadi za maneno<br>• Seti ya projekta<br>• Kinasa sauti | • Maswali na majibu<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano | 12 |

| STADI | MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | iii. Kuunda silabi kutokana na herufi.<br>iv. Kuunda maneno kutokana na silabi. | | | | |
| | 4.2 Hati | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kuandika maneno kwa kuunganisha silabi.<br>ii. Kuandika sentensi fupi kwa kuunganisha maneno. | • Maswali na majibu<br>• Nyimbo<br>• Michezo<br>• Fikiri jozisha shirikisha<br>• Majigambo | • Chati ya nakshi nane za msingi<br>• Chati ya herufi kubwa na ndogo<br>• Kadi za herufi kubwa na ndogo<br>• Chati za maneno<br>• Chati ya sentensi<br>• Modeli ya | • Maswali na majibu<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano | 12 |

| STADI | MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | iii. Kunukuu hati kwa kuzingatia kanuni za uandishi. | | kipaza sauti | | |
| | 4.3 Imla ya sentensi fupi (isiyozidi maneno manane) | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kubainisha maneno teule.<br>ii. Kuandika sentensi fupi.<br>iii. Kusoma sentensi . | • Imla<br>• Maswali na majibu<br>• Mazoezi | • Kinasa sauti<br>• Matini ya sentensi<br>• Kadi za maneno | • Maswali na majibu<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano | 10 |

| STADI | MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 4.4 Uandishi wa aya fupi | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kubainisha alama ya kituo kikubwa(.) na alama ya kuuliza(?) katika uandishi.<br>ii. Kupanga maneno kuwa sentensi fupi.<br>iii. Kuandika aya fupi. | • Fikiri jozisha shirikisha<br>• Michezo<br>• Matembezi ukumbini<br>• Majadiliano<br>• Onesho mbinu | • Chati ya alama za uandishi<br>• Kadi za maneno<br>• Ubao wa sentensi<br>• Matini ya aya fupi | • Maswali na majibu<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano | 16 |
| | 4.5 Kuandika nambari kwa maneno (1- | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kuainisha | • Onesho mbinu<br>• Fikiri jozisha shirikisha<br>• Michezo | • Kadi za nambari<br>• Kadi za maneno | • Maswali na majibu<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya | 12 |

| STADI | MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 150) | nambari kwa tarakimu.<br>ii. Kubainisha nambari kwa maneno.<br>iii. Kulinganisha nambari kwa tarakimu na maneno.<br>iv. Kuandika nambari kwa maneno. | • Matembezi ukumbini | • Kapu la kadi za maneno<br>• Kapu la kadi za nambari | mkono<br>• Majadiliano | |
| | **5. SARUFI**<br>5.1 Majina (ya watu, vitu na pahala) | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kuainisha majina | • Fikiri jozisha shirikisha<br>• Onesho mbinu<br>• Maswali na majibu<br>• Michezo | • Kadi za majina<br>• Kadi za picha na maneno<br>• Video<br>• Televisheni, | • Maswali na majibu<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono | 14 |

| STADI | MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | katika sentensi.<br>ii. Kubainisha majina katika aya fupi fupi.<br>iii. Kutunga sentensi kwa kutumia majina. | • Majadiliano | Flashi<br>• Seti ya DVD<br>• Kadi za sentensi<br>• Seti ya projekta<br>• Kinasa sauti | • Majadiliano<br>• Chemsha bongo | |
| | 5.2 Umoja na wingi | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kuelezea majina ya watu, vitu na pahala.<br>ii. Kubainisha majina yenye sifa za umoja na wingi. | • Michezo<br>• Fikiri jozisha shirikisha<br>• Maswali na majibu<br>• Majadiliano | • Kadi za maneno<br>• Ubao wa sentensi<br>• Kapu la kadi za majina<br>• Rangi<br>• Manila | • Maswali na majibu<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano | 12 |

| STADI | MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | iii. Kubadilisha majina ya umoja kwenda wingi na wingi kwenda umoja.<br>iv. Kuchora picha za vitu vyenye majina ya umoja na wingi. | | | | |
| | 5.3 Neno Kinyume | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kubainisha kinyume cha maneno.<br>ii. Kubadilisha maneno kuwa | • Fikiri jozisha shirikisha<br>• Onesho mbinu<br>• Michezo<br>• Majadiliano<br>• Maswali na majibu<br>• Matembezi ukumbini | • Kadi za maneno<br>• Kapu la kadi za maneno<br>• Chati ya maneno kinyume | • Maswali na majibu<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano | 10 |

| STADI | MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | kinyume. | | | | |
| KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA | **6. FASIHI SIMULIZI**<br><br>6.1 Vitendawili | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kubainisha vitendawili vilivyomo katika mazingira yao.<br>ii. Kufuata hatua za kutega na kutegua vitendawili.<br>iii. Kutega na kutegua vitendawili. | • Michezo<br>• Bungua bongo<br>• Onesho mbinu<br>• Majadiliano | • Kadi za vitendawili<br>• Kadi za picha<br>• Seti ya DVD<br>• Kinasa sauti<br>• Seti ya projekta | • Maswali na majibu<br>• Ugunduzi<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano<br>• Chemsha bongo | 12 |
| | 6.2 Nyimbo | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:**<br>i. Kubainisha | • Onesho mbinu<br>• Maswali na majibu<br>• Majadiliano<br>• Fikiri jozisha | • Picha<br>• Seti ya projekta<br>• Kinasa sauti<br>• Vitabu vya | • Maswali na majibu<br>• Ugunduzi<br>• Uchunguzi | 12 |

| STADI | MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | nyimbo zenye maadili zilizomo katika mazingira yake.<br>ii. Kuimba nyimbo fupi zenye maadili zilizomo katika mazingira yake.<br>iii. Kueleza mafunzo yanayotokana na nyimbo. | shirikisha | nyimbo<br>• Nakala za nyimbo | • Ishara ya mkono<br>• Majadiliano | |

# DARASA LA II

## Matokeo ya Jumla ya Kujifunza kwa Darasa la II

Katika kujifunza somo la Kiswahili kwa darasa la pili mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-

1. Kusikiliza na kufuata maelekezo kwa usahihi.
2. Kusoma na kuandika sentensi na aya fupi kwa usahihi.
3. Kusoma na kuandika maneno na sentensi na aya fupi kwa usahihi.
4. Kutumia maktaba kusoma vitabu na machapisho mengine.
5. Kutumia vipengele vya msingi vya sarufi ya Kiswahili katika kuzungumza na kuandika.
6. Kutumia methali na ngano katika kujenga udadisi

## DARASA LA PILI

| STADI | MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA | **1. MAWASILIANO**<br><br>1.1 Maelekezo | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa: -**<br>i. Kubainisha msamiati wa maelekezo uliyomo katika habari aliyoisoma.<br>ii. Kubainisha maelekezo yaliyomo katika hadithi.<br>iii. Kutoa maelekezo. | • Maswali na majibu<br>• Fikiri jozisha shirikisha<br>• Majadiliano<br>• Onesho mbinu<br>• Nyimbo<br>• Michezo | • Vitabu vya hadithi<br>• Kadi za matendo ya maelekezo<br>• Picha za matendo ya maelekezo | • Maswali na majibu<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano<br>• Usahihishaji rika | 14 |
| | 1.2 Kuitambulisha familia (baba, mama, dada na kaka) | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-** | • Maswali na majibu<br>• Nyimbo<br>• Onesho mbinu<br>• Michezo | • Mti wa familia<br>• Kadi za maneno<br>• Picha za | • Maswali na majibu<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya | 16 |

| STADI | MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | i. Kuainisha watu wanaojenga familia.<br>ii. Kueleza watu wa familia yake.<br>iii. Kuchora picha za watu wa familia yake.<br>iv. Kuelezea majukumu ya watu wa familia yake. | | majukumu ya wanafamilia<br>• Rangi | mkono<br>• Majadiliano<br>• Mkoba wa kazi | |
| | 1.3 Kutambulisha watu wengine (bibi, babu, shangazi na mjomba) | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kuainisha watu wengine wa | • Maswali na majibu<br>• Nyimbo<br>• Michezo<br>• Onesho mbinu<br>• Matembezi ukumbini | • Kadi za maneno<br>• Chati ya majina ya watu na kazi zao<br>• Manila | • Maswali na majibu<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano | 16 |

| STADI | MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | familia.<br>ii. Kueleza watu wengine wa familia.<br>iii. Kufafanua majukumu ya watu wengine wa familia. | | • Kalamu rashasha | | |

| STADI | MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **KUSOMA** | **2. USOMAJI**<br>2.1 Kusoma kwa mazoezi | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kuelezea alama za uandishi.<br>ii. Kukariri sentensi kwa kufuata alama za uandishi.<br>iii. Kusoma kwa kuzingatia alama za uandishi. | • Matembezi ukumbini<br>• Michezo<br>• Mazoezi<br>• Onesho mbinu | • Kadi za sentensi<br>• Chati za alama za uandishi | • Maswali na majibu<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano | 16 |
| | 2.2 Kusoma kwa ufahamu (habari fupi isiyozidi maneno 200) | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kuainisha msamiati teule | • Maswali na majibu<br>• Majadiliano<br>• Fikiri jozisha shirikisha | • Matini fupi<br>• Kadi za maneno teule<br>• Karatasi za maandishi makubwa | • Maswali na majibu<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano | 16 |

| STADI | MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | uliotumika katika habari.<br>ii. Kueleza mafunzo yaliyomo katika habari.<br>iii. Kufupisha habari. | | | • Mkoba wa kazi | |
| | 2.3 Kusoma nambari (151-200) | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kutamka nambari kwa maneno.<br>ii. Kuainisha nambari kwa maneno. | • Michezo<br>• Matembezi ukumbini<br>• Fikiri jozisha shirikisha<br>• Majibizano | • Kadi za maneno<br>• Kadi za nambari<br>• Kadi za maneno na nambari | • Maswali na majibu<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano | 16 |

| STADI | MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
| --- | --- | --- | --- | --- | --- | --- |
| | | iii. Kulinganisha nambari na maneno ya nambari. | | | | |
| | **3. MAKTABA**<br>3.1 Maktaba ya skuli | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kubainisha sababu za kuanzishwa maktaba ya skuli.<br>ii. Kueleza vifaa vinavyopatikana katika maktaba ya skuli.<br>iii. Kutumia maktaba ya skuli kusoma | • Bungua bongo<br>• Ziara ya kimasomo<br>• Onesho mbinu<br>• Fikiri jozisha shirikisha<br>• Maswali na majibu | • Vitabu vya picha<br>• Vitabu vya maneno<br>• Makala<br>• Sampuli ya kadi zinazotumika maktaba | • Maswali na majibu<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano<br>• Mkoba wa kazi<br>• Orodha hakiki | 10 |

| STADI | MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | vitabu. | | | | |
| | 3.2 Maktaba ya darasa | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kubainisha vifaa vya kusomea katika maktaba ya darasa.<br>ii. Kupanga vifaa vya kusomea baada ya matumizi.<br>iii. Kuelezea njia za kuhifadhi vifaa vya kusomea katika maktaba ya | • Onesho mbinu<br>• Fikiri jozisha shirikisha | • Vijarida<br>• Vijarida vya nukta nundu<br>• Vitabu<br>• Kadi za maandishi makubwa<br>• Kadi za maneno<br>• Kadi za sentensi | • Maswali na majibu<br>• Ugunduzi<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano | 18 |

| STADI | MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | darasa. | | | | |
| KUANDIKA | **4. UANDISHI**<br>4.1 Hati (isiyozidi sentensi tano) | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kubainisha alama za uandishi.<br>ii. Kueleza matumizi ya alama za uandishi.<br>iii. Kuandika hati zinazosomeka kwa kuzingatia alama za uandishi. | • Onesho mbinu<br>• Maswali na majibu<br>• Nyimbo | • Matini<br>• Chati ya alama za uandishi<br>• Kadi za sentensi | • Maswali na majibu<br>• Usahihishaji rika<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano | 10 |
| | 4.2 Imla (aya isiyozidi | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-** | • Onesho mbinu<br>• Imla | • Kinasa sauti<br>• Matini | • Maswali na majibu | 12 |

| STADI | MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | sentensi tano) | i. Kubainisha maneno teule.<br>ii. Kuandika sentensi fupi fupi.<br>iii. Kuandika aya fupi. | • Maswali na majibu<br>• Mazoezi<br>• Majadiliano | • Chati yenye sentensi fupi fupi<br>• Kadi za maneno | • Usahihishaji rika<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano | |
| | 4.3 Utungaji (aya ndefu isiyozidi sentensi saba) | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kubainisha alama za uandishi.<br>ii. Kupanga maneno kuunda sentensi.<br>iii. Kutunga aya | • Majadiliano<br>• Michezo<br>• Nyimbo<br>• Maswali na majibu | • Kadi za sentensi<br>• Chati ya alama za uandishi<br>• Matini | • Maswali na majibu<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano<br>• Chemsha bongo | 12 |

| STADI | MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | ndefu. | | | | |
| | 4.4 Utungaji (Insha ya picha) | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kuchunguza picha.<br>ii. Kubainisha hatua za utungaji wa insha ya picha.<br>iii. Kutunga insha ya picha. | • Michezo<br>• Maswali na majibu<br>• Majadiliano<br>• uchunguzi | • Sampuli ya insha<br>• Kadi za sentensi<br>• Chati ya picha | • Maswali na majibu<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano<br>• Chemsha bongo | 14 |
| | 4.5 Kuandika nambari kwa maneno (151-200) | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kuainisha nambari kwa maneno. | • Michezo<br>• Onesho mbinu<br>• Majadiliano<br>• Fikiri jozisha shirikisha<br>• Matembezi ukumbini | • Kapu la kadi za nambari<br>• Chati ya nambari<br>• Kadi za maneno ya nambari | • Maswali na maj<br>• Usahihishaji rik<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkon<br>• Majadiliano<br>• Mkoba wa kazi | 14 |

| STADI | MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | ii. Kulinganisha nambari na maneno ya nambari.<br>iii. Kuandika nambari kwa maneno. | | • Ubao wa sentensi | | |
| | **5. SARUFI**<br>5.1 Majina (ya pekee na ya kawaida) | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kubainisha majina.<br>ii. Kuainisha majina ya pekee na majina ya kawaida.<br>iii. Kutumia majina ya pekee na ya | • Onesho mbinu<br>• Michezo<br>• Nyimbo<br>• Majadiliano<br>• Maswali na majibu<br>• Fikiri jozisha shirikisha | • Chati ya majina<br>• Kadi za majina<br>• Matini | • Maswali na maj<br>• Usahihishaji rik<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano<br>• Kadi mrejesho | 12 |

| STADI | MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | kawaida katika utungaji wa sentensi. | | | | |
| | 5.2 Nyakati za msingi (wakati uliopo, uliopita na ujao) | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kubainisha maneno yanayooneshа nyakati katika sentensi.<br>ii. Kubainisha matendo yanayoonesha wakati uliopo, uliopita na ujao.<br>iii. Kutumia viambishi vya wakati | • Majadiliano<br>• Maswali na majibu<br>• Michezo<br>• Fikiri jozisha shirikisha<br>• Mazoezi<br>• Nyimbo | • Kadi za maneno ya wakati uliopo, uliopita na ujao<br>• Picha za matendo ya wakati uliopo, uliopita na ujao<br>• Matini | • Maswali na majibu<br>• Usahihishaji rika<br>• Mkoba wa kazi<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano | 16 |

| STADI | MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | uliopo, uliopita na ujao katika sentensi. | | | | |
| | 5.3 Nafsi | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kuainisha maneno yanayoonesha nafsi.<br>ii. Kubadilisha nafsi kutoka hali ya umoja kwenda wingi.<br>iii. Kutumia nafsi za umoja na wingi katika utungaji wa | • Maswali na majibu<br>• Michezo<br>• Nyimbo<br>• Matembezi ukumbini | • Kadi za maneno<br>• Chati ya sentensi zinazoonesha nafsi<br>• Vikaragosi<br>• Matini | • Maswali na majibu<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano<br>• Mkoba wa kazi<br>• Tathmini binafsi | 12 |

| STADI | MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | sentensi. | | | | |
| | **6. FASIHI SIMULIZI**<br>6.1 Methali | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kubainisha methali zilizomo katika jamii.<br>ii. Kuchambua methali zilizomo katika hadithi/makala.<br>iii. Kuelezea mafunzo yanayotokana na methali. | • Hadithi<br>• Maswali na Majibu<br>• Fikiri jozisha shirikisha<br>• Majadiliano<br>• Michezo | • Chati za methali<br>• Makala<br>• Kadi zinazoonesha methali | • Maswali na majibu<br>• Usahihishaji rika<br>• Mawazo mkufu<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano<br>• uchunguzi | 14 |
| | 6.2 Ngano | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kusimulia | • Hadithi<br>• Maswali na majibu<br>• Michezo<br>• Igizo dhima | • Vitabu vya hadithi<br>• Vikaragosi<br>• Kinasa sauti | • Maswali na majibu<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya | 14 |

| STADI | MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | ngano zilizomo katika jamii.<br>ii. Kubainisha wahusika waliyomo katika ngano na sifa zao.<br>iii. Kuelezea mafunzo yaliyomo katika ngano. | • Majadiliano<br>• Kumualika mgeni | • Picha<br>• Chati | mkono<br>• Majadiliano<br>• Kadi mrejesho<br>• Mkoba wa kazi | |

# DARASA LA III

## DARASA LA III

### Matokeo ya Jumla ya Kujifunza kwa Darasa la III

Katika kujifunza somo la Kiswahili kwa darasa la tatu mwanafunzi aoneshe uwezo wa:

1. Kusoma na kuandika matini, vitabu na machapisho mengine ya Kiswahili kwa maarifa na burudani.
2. Kutumia vipengele vya msingi vya sarufi ya Kiswahili katika kuzungumza na kuandika.
3. Kutumia mashairi na visasili kujenga udadisi.

## DARASA LA TATU

| STADI | MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA** | **1. MAWASILIANO**<br>1.1 Ishara | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kubainisha mawasiliano ya ishara.<br>ii. Kujadili ishara za mawasiliano.<br>iii. Kutumia ishara katika mawasiliano. | • Maswali na majibu<br>• Fikiri jozisha shirikisha<br>• Majadiliano<br>• Kisa mafunzo<br>• Michezo<br>• Nyimbo | • Projekta<br>• Video<br>• Seti ya DVD<br>• Kinasa sauti<br>• Redio | • Maswali na majibu<br>• Ugunduzi<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano<br>• Chemsha bongo | 10 |
| | 1.2 Mazungumzo | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kufafanua sifa za mazungumzo<br>ii. Kueleza aina | • Maswali na majibu<br>• Usimulizi wa hadithi<br>• Michezo<br>• Igizo dhima<br>• Dayalojia | • Picha za matukio<br>• Redio<br>• Kadi za picha<br>• Seti ya projekta<br>• Seti ya video<br>• Seti ya DVD | • Maswali na majibu<br>• Ugunduzi<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano<br>• Chemsha | 14 |

| STADI | MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | za mazungumzo<br>iii. Kuwasiliana kwa kuzungumza. | | | bongo | |
| | 1.3 Maandishi | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kuainisha mawasiliano ya maandishi.<br>ii. Kueleza aina za mawasiliano ya maandishi.<br>iii. Kuwasiliana kwa maandishi. | • Maswali na majibu<br>• Matembezi ukumbini<br>• Igizo dhima<br>• Nyimbo | • Shajara<br>• Kalamu<br>• Simu<br>• Simu upepo<br>• Orodha ya maswali<br>• Kadi | • Maswali na majibu<br>• Ugunduzi<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano<br>• Chemsha bongo | 12 |

| STADI | MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **KUSOMA** | **2. USOMAJI**<br><br>2.1 Kusoma kwa Mazoezi (habari fupi isiyozidi maneno 300) | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kuainisha alama za uandishi.<br>ii. Kueleza matumizi ya alama za uandishi.<br>iii. Kusoma kwa kasi kwa kuzingatia alama za uandishi. | • Onesho mbinu<br>• Michezo<br>• Mbio za vijiti | • Chati ya alama za uandishi<br>• Matini<br>• Vitabu vya hadithi<br>• Makala<br>• Magazeti<br>• Vipeperushi | • Maswali na majibu<br>• Ugunduzi<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano<br>• Chemsha bongo | 16 |
| | 2.2 Kusoma kwa ufahamu (habari fupi isiyozidi maneno 300 dawa za | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kubainisha maneno teule | • Michezo<br>• Maswali na majibu<br>• Fikiri jozisha shirikisha<br>• Majadiliano | • Matini<br>• Matini ya nukta nundu<br>• vitabu vya hadithi<br>• Magazeti | • Maswali na majibu<br>• Ugunduzi<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono | 16 |

| STADI | MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | kulevya). | ya habari.<br>ii. Kujibu maswali kutokana na habari.<br>iii. Kufupisha habari. | | • Kadi za maneno<br>• Orodha ya maswali | • Majadiliano<br>• Chemsha bongo | |
| | 2.3 Kusoma nambari kwa maneno (201-300) | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kubainisha nambari kwa maneno.<br>ii. Kulinganisha nambari na maneno.<br>iii. Kusoma maneno ya nambari. | • Michezo<br>• Matembezi ukumbini<br>• Fikiri jozisha shirikisha<br>• Majadiliano<br>• Maswali na majibu | • Kadi za maneno<br>• Kadi za nambari<br>• Kadi za maneno na nambari<br>• Vikaragosi<br>• Orodha ya maswali | • Maswali na majibu<br>• Ugunduzi<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano<br>• Chemsha bongo | 16 |

| STADI | MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2.4 Matumizi ya maktaba | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kuainisha sehemu za maktaba.<br>ii. Kubainisha alama zinazotumika maktaba.<br>iii. Kutumia vifaa vinavyopatika na maktaba katika sehemu ya kusomea watoto. | • Ziara ya kimasomo<br>• Onesho mbinu<br>• Fikiri jozisha shirikisha<br>• Maswali na Majibu | • Vitabu<br>• Maktaba<br>• Majarida | • Maswali na majibu<br>• Ugunduzi<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano<br>• Chemsha bongo | 14 |

| STADI | MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| KUANDIKA | **3. UANDISHI**<br><br>3.1 Hati (maneno yasiyozidi mia moja 100) | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kuchambua habari fupi.<br>ii. Kuelezea matumizi ya alama za uandishi.<br>iii. Kuandika hati zinazosomeka kwa urahisi. | • Onesho mbinu<br>• Nyimbo<br>• Mazoezi | • Kadi za sentensi<br>• Maandishi makubwa<br>• Kadi za alama za uandishi<br>• Matini<br>• Hadithi<br>• Seti ya projekta<br>• Kinasa sauti | • Maswali na majibu<br>• Ugunduzi<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano<br>• Chemsha bongo | 14 |
| | 3.2 Imla (habari fupi isiyozidi maneno hamsini 50) | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kuainisha maneno teule.<br>ii. Kubainisha hatua za | • Onesho mbinu<br>• Maswali na majibu<br>• Michezo<br>• Imla | • Kinasa sauti<br>• Matini ya habari<br>• Chati ya alama za uandishi<br>• Seti ya projekta<br>• Kinasa sauti | • Maswali na majibu<br>• Ugunduzi<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano<br>• Chemsha | 14 |

| STADI | MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
| --- | --- | --- | --- | --- | --- | --- |
| | | uandishi wa imla.<br>iii. Kuandika imla fupi kwa kuzingatia alama za uandishi. | | | bongo | |
| | 3.3 Utungaji wa insha fupi za mtiririko wa picha. | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kuainisha aina za insha.<br>ii. Kubainisha hatua za utungaji.<br>iii. Kuandika insha kwa mtiririko wa | • Bungua bongo<br>• Fikiri jozisha shirikisha<br>• Matembezi ukumbini<br>• Majadiliano<br>• Maswali na majibu | • Ubao wa sentensi<br>• Picha mtiririko<br>• Picha mguso mtiririko<br>• Seti ya video<br>• Seti ya DVD<br>• Vitu halisi<br>• Chati za sentensi<br>• Projekta | • Maswali na majibu<br>• Ugunduzi<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano<br>• Chemsha bongo | 14 |

| STADI | MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | picha. | | | | |
| | 3.4 Kuandika nambari kwa maneno (1-300) | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kubainisha maneno ya nambari teule.<br>ii. Kujadili maneno ya nambari teule.<br>iii. Kuandika nambari na maneno ya nambari. | • Fikiri jozisha shirikisha<br>• Michezo<br>• Onesho mbinu<br>• Igizo dhima<br>• Maswali na majibu<br>• Majadiliano<br>• Majigambo<br>• Nyimbo<br>• Hadithi | • Kapu la maneno<br>• Kapu la kadi za nambari<br>• Vikaragosi<br>• Orodha ya maswali<br>• Karatasi ya maandishi makubwa | • Maswali na majibu<br>• Ugunduzi<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono<br>• Majadiliano<br>• Chemsha bongo | 14 |
| | **4. SARUFI**<br>4.1 Nyakati za msingi (wakati uliopo, uliopita na ujao). | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:-**<br>i. Kubainisha nyakati. | • Fikiri jozisha shirikisha<br>• Onesho mbinu<br>• Maswali na majibu<br>• Majadiliano<br>• Matembezi ukumbini | • Kadi za vitenzi<br>• Picha<br>• Picha ya mguso<br>• Seti za video<br>• Seti za DVD<br>• Kadi za | • Maswali na majibu<br>• Ugunduzi<br>• Uchunguzi<br>• Ishara ya mkono | 14 |